Mungu Roho Mtakatifu

“Mungu Roho Mtakatifu wa milele alikuwa mtendani pamoja na Baba na Mwana katika Uumbaji, katika Yesu kufanyika mwili na katika ukombozi. Aliwavuvia waandishi wa Maandiko Matakatifu. Alijaza maisha ya Yesu Kristo na uwezo. Huwavuta na kuasadikisha wanadamu; na wale wanaoitikia huwafanya upya na kuwabadilisha katika sura ya Mungu. Alipelekwa na Baba na Mwana ili kuwa siku zote pamoja na watoto wake, hueneza karama za Roho kwa kanisa., na kuwapa uwezo wa kumshuhudia Kristo, na kwa ulinganifu na Maandiko Matakatifu hongoza katika kweli yote.” (Mwa.1:1, 2; Luk.1:35; 4:18; Mdo.10:38; 2Pet.1:21; 2Kor.3:18; Efe.4:11, 12; Mdo. 1:8; Yoh.4:16-18, 26; 15:26, 27; 16:7-13)

Ijapokuwa kusulubiwa kuliwachanganya, kuwanyong’onyeza, na kuwatisha wafuasi wa Kristo, ufufuo ulileta asubuhi katika maisha yao. Kristo alipovunja vifungo vya kifo, ufalme wa Mungu ulileta nuru katika mioyo yao. Sasa moto usiozimika uliwaka mioyoni mwao. Tofauti ambazo wiki chache zilizopita zilileta kuta za vipingamizi, ziliyeyuka. Waliungamiana makosa wao kwa wao na kufungua mioyo yao kikamilifu kumpokea Yesu, mfalme wao aliyepaa. Umoja wa kundi hili ambalo awali lilikuwa limetawanyika, uliongezeka kadiri walivyotumia wakati wao katika maombi. Siku moja isiyosahaulika, walipokuwa wakimsifu Mungu, ndipo kelele za ngurumo za mvua ya dhoruba ilipowafikia. Kana kwamba mwako ulio mioyoni mwao unaonekana, miale ya moto iliwashukia kila moja wao. Kama moto unaowaka, Roho Mtakatifu aliwafikia.

Wakiwa wamejazwa Roho Mtakatifu wafuasi hawa hawakuweza kuficha upendo wao wa dhati na furaha yao katika Yesu. Kwa hamu kubwa na kwa uwazi, walianza kuhubiri habari njema za wokovu. Wakishangazwa kwa sauti, umati wa watu ukaliendea jengo walimokuwamo. Wakiwa wamechanganyikiwa na kujawa mshangao, walisikia Wagalilaya wakisema habari njema za Yesu katika lugha zao wenyewe. “Hatuelewi”, baadhi yao walisema, wengine wakajaribu kupenyeza uvumi, “wamelewa”. “Siyo hivyo”, Petro akapaza sauti yake mbele ya umati, “sasa ni saa tatu za asubuhi, haiwezekani kukawa na kulewa”. Mlichosikia na kukiona kikitokea ni kwa sababu Yesu Kristo aliyefufuka ameinuliwa na kuketi mkono wa kuume wa Mungu na amegawa Roho Mtakatifu. (Mdo. 2).

Roho Mtakatifu ni Nani?

Biblia hufunua kuwa Roho Mtakatifu ni nafsi na siyo nishati isiyo nafsi. Kauli kama “ilimpendeza Roho Mtakatifu na sisi” (Mdo.15:28), hufunua kuwa waumini wa awali walimwona Yeye kuwa nafsi. Kristo naye alimtaja kuwa ni nafsi “atanitukuza mimi kwa kuwa atatwaa katika yangu na kuwapasha habari” (Yoh.16:14). Maandiko yakielezea Utatu Mtakatifu, humtaja Roho Mtakatifu kuwa nafsi (Mt.28:19; 2Kor.13:14). Roho Mtakatifu ni nafsi kwa kuwa hushindana (Mwa.6:3), hufundisha (Luk.12:12), husadikisha (Yoh.16:8), huendesha shughuli za kanisa (Mdo. 13:2), husaidia kuombea (Rum.8:26), huvuvia (2Pet.1:21) na kutakasa (1:1:2). Matendo haya, hayafanywi na nguvu ya Mungu bali na Nafsi ya Roho Mtakatifu.

Roho Mtakatifu Kwa Uhalisi ni Mungu

Maandiko Matakatifu humhesabu Roho Mtakatifu kuwa ni Mungu. Petro alimwambia Anania ‘kwa kumwambia uwongo Roho Mtakatifu alikuwa hamwambii uongo mwanadamu

bali Mungu' (Mdo. 5:3, 4). Yesu aliitaja dhambi isiyosameheka kuwa ni ya kumkufuru Roho Mtakatifu (Matt.12:31, 32). Hili litakuwa kweli ikiwa tu, Roho Mtakatifu ni Mungu.
Biblia huzielezea sifa za Uungu kwa Roho Mtakatifu. Ni uzima "Roho wa uzima" (Rum.8:2). Ni Kweli – "Roho wa Kweli" (Yoh.16:13), upendo wa Roho (Rum.15:30), na Roho Mtakatifu wa Mungu (Efe.4:30), huonesha upendo na utakatifu ni sehemu ya asili yake.

Roho Mtakatifu hupatikana wakati wote na mahali pote. Hugawa karama za roho kadiri apendavyo (1Kor.12:11). Yupo wakati wote. "Atakaa na watu wake milele" (Yoh.14:16). Hakuna ambaye aweza kukwepa mvuto wake (Zab.139:7-10). Roho Mtakatifu anajua yote kwa sababu aweza kuyachunguza mafumbo ya Mungu kwa sababu anayajua (1Kor.2:10, 11).

Kazi za Mungu pia zinahusishwa na Roho Mtakatifu. Uumbaji na ufufuo vinamhusisha Yeye (Ayu. 33:4). "Waipeleka Roho yako, wanaumbwa, (Zab.104:30). Roho aliyemfufua Kristo katika wafu, ataihuisha miili iliyo katika hali ya kufa. (Rum.8:11). Ni Mungu apatikanaye wakati wote ndiye angeweza kutenda muujiza wa wa kumleta Mungu Kristo kwa mwanadamu - Mariam. Siku ya Pentekoste, Roho alimfanya Mungu–Mwanadamu pekee Yesu, aweze kupatikana katika ulimwengu wote kwa wanaopenda kumpokea. Roho Mtakatifu yuko sawa na Baba na Yesu katika kanuni ya ubatizo (Mt.28:19) na katika baraka ya mitume (2Kor.13:14) na katika kufunua karama za roho (1Kor.13:14).

Roho Mtakatifu na Utatu Mtakatifu
Tangu milele Mungu Roho Mtakatifu aliishi katika Utatu Mtakatifu akiwa wa tatu. Pamoja na kuwa sawa, kuna mgawano wa majukumu katika Utatu Mtakatifu. (Angalia somo la Mungu Mwana). Ukweli kumhusu Roho Mtakatifu hueleweka vema kupitia Yesu Kristo. Matendo yake katika historia, humwelekea Kristo katika utume wa wokovu. Alihusika katika kuzaliwa kwa Yesu (Luk.1:35). Alithibitisha utume wake katika ubatizo (Mt.3:16, 17) and kuleta mafao ya kafara ya Kristo na ufufuo kwa wanadamu (Rum.8:11). Anaoneka kuwa Mtekelezaji. Baba alipomtoa Yesu kwa ulimwengu (Yoh.3:16), Roho aliwezesha mimba ifanyizwe (Mt.1:18-20), akaufanya mpango utekelezeke. Kuhusika kwa Roho katika Uumbaji, kunaonekana kwa kuweko kwake tangu mwanzo (Mwa.1:2). Asili ya uhai na kuudumisha kunategemea utendaji wake. (Ayu.34:14, 15; cf. 33:4). Tunauona utendaji wa Roho katika watu binafsi, anapowaumba wawe watoto wa Mungu.

Roho Aliyeahidiwa
Tuliumbwa ili Roho Mtakatifu apate maskani katika miili yetu (1Kor.3:16). Adamu na Hawa walijitenga na Edeni na Roho akaaye ndani, hadi Mungu akasema wakati wa gharika "Roho yangu haitashindana na mwanadamu milele (Mwa.6:3). Katika Agano la Kale aliwapatia baadhi ya watu kufanya kazi maalum (Hes.24:2; Amu.6:34; 1Sam.10:6). Nyakati kadhaa huwa ndani ya watu (Kut. 31:3; Isa. 63:11). Pasipo shaka waumini wana ufahamu wa kuwapo kwake, hata hivyo ilitabiriwa kumwagwa kwa Roho Mtakatifu kwa wote wenye mwili (Yoe.2:28), wakati ambao udhihirisho wa Roho utaleta enzi mpya.

Wakati ulimwengu ulipokuwa kwenye mikono ya mnyang'anyi umwagaji wa Roho Mtakatifu ulipaswa kusubiri. Akionyesha utume wa Kristo, Yohana Mbatizaji alisema kuwa Yesu atabatiza kwa Roho Mtakatifu (Mt.3:11). Injili hazisemi kuwa Yesu alibatiza kwa Roho. Lakini kabla ya kifo chake, Yesu aliahidi wafuasi wake kuwa atamwomba Baba awapatie Msaidizi mwingine, akae nao milele, Roho wa Kweli. (Yoh.14:16, 17). Je, ubatizo ulipatikana

msalabani? Hapana. Ni mpaka baada ya kufufuka kwake ndipo alipowapa Roho Mtakatifu (Yoh.20:22).

Aliwaambia wasubiri Yerusalemu, hadi wapatiwe uwezo (Luk.24:49). Roho aliyepokewa, angewezesha wafuasi kuwa mashahidi hadi mwisho wa nchi. (Mdo.1:8). Yohana alidokeza Roho hakutolewa kabla ya Yesu kutukuzwa (Yoh.7:39). Enzi mpya ilianza baada ya Yesu kuketi mkono wa kuume wa Mungu. Petro alisema, alimwaga Roho Mtakatifu (Mdo.2:33) kwa waliotazamia kwa hamu kutimizwa kwa jambo hili wakiwa wamoja (Mdo.1:5, 14). Katika siku ya Pentekoste, siku hamsini tangu Kalvari, enzi mpya ilianza: "Kukaja ghafla toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu, ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote, waliyokuwa wameketi. Kukawatokea ndimi zilizogawanyikana, kama ndimi za moto uliowakalia kila mmoja wao. Wote wakajazwa Roho Mtakatifu" (Mdo.2:2-4). Utume wa Yesu na Utume wa Roho Mtakatifu havikuingiliana. Ujazo wa Roho Mtakatifu haukutimilika kwa kiwango kikamilifu hadi Yesu alipokamilisha utume wake. Na kwa upande mwingine, Yesu alizaliwa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu (Mt.1:8-21), alibatizwa na Roho Mtakatifu (Mk.1:9,
10), Aliongozwa na Roho (Luk.4:1), alitenda miujiza kwa Roho Mtakatifu (Mt.12:24-32), akajitoa mwenyewe Kalvari kwa Roho Mtakatifu (Ebr.9:14, 15) na kwa sehemu, alifufuliwa na Roho Mtakatifu (Rum.8:11). Yesu alikuwa wa kwanza kujazwa kwa ujazo wote, Roho Mtakatifu. Na ukweli wa ajabu ni kwamba, Yuko tayari kumjaza yeyote Roho wake, mtu anayemhitaji kwa bidii.

Utume wa Roho Mtakatifu
Usiku kabla ya kifo cha Kristo, maneno yake kuhusu kuondoka kwake katika kipindi kifupi kijacho, yaliwafanya wanafunzi wake wafadhaike. Haraka aliwaahidi kuwapa Roho Mtakatifu na hatawaacha yatima. (Yoh.14:18)

Asili ya Utume
Agano Jipya humdhihirisha Roho Mtakatifu katika njia maalum. Anaitwa Roho wa Yesu (Mdo.16:7), Roho wa Mwana (Gal.4:6), Roho wa Mungu (Rum.8:9), Roho wa Kristo (Rum.8:9; 1Pet.1:11) na Roho wa Yesu Kristo (Fil.1:19). Ni nani aliyeanzisha utume wa Roho Mtakatifu, ni Yesu Kristo au Mungu Baba?

Yesu alipodhihirisha asili ya utume wa Roho Mtakatifu kwa ulimwengu uliopotea, alitaja vyanzo viwili. Kwanza kwa Baba (14:16; cf 15:26). Ubatizo wa Roho Mtakatifu ni ahadi ya Baba (Mdo.1:4). Pili, Yesu alijirejea Yeye kama chanzo. Nitamtuma kwenu (Yoh.16:7). Hivyo Roho Mtakatifu alitoka kwa Baba na kwa Yesu.

Utume wake kwa Ulimwengu. Twaweza kukubali Ubwana wa Kristo kwa kupitia Roho Mtakatifu pekee (1Kor.12:3). Twahakikishiwa kwa Roho Mtakatifu kuwa Nuru ya Kweli yamwangazia kila mtu ajaye ulimwenguni (Yoh.1:9). Utume wake ni kusadikisha ulimwengu juu ya dhambi na haki na hukumu (Yoh.16:8). Kwanza anatusadikisha dhambi kubwa ya kutomwamini Yesu (Yoh.16:9). Pili Roho hutushurutisha tuipokee haki ya Kristo. Tunapotubu twazaliwa upya kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu (Yoh.3:5). Sasa maisha yetu huwa mapya kwa kuwa tumekuwa maskani ya Roho Mtakatifu.

Utume wake kwa Waumini. Wingi wa mafungu ya Biblia kuhusu utendaji wa Roho Mtakatifu unahusiana na uhusiano wake na watu wa Mungu. Mvuto wake wa kutakasa (1Pet.1:2) lakini haiwezekani kuendelea kuwa naye pasipo kutimiza masharti kadha wa

kadha. Petro anasema Mungu amemtoa Roho kwa wale wanaoendelea kumtii (Mdo. 5:32). Hivyo waumini wanaonywa wasije wakampinga, wakamhuzunisha, wakamzima Roho Mtakatifu. (Mdo7:51, Efe.4:30; 1Thes.519)

1. ***Husaidia waumini***: Alipomtambulisha Roho, Kristo alisema atakuwa Msaidizi (Yoh.14:16). Tunaonywa tusitende dhambi na kama tukitenda dhambi, tunaye Mwombezi kwa Baba. (1Yoh.2:1). Hivyo, Roho hutuongoza kwa Kristo na neema yake. Hiyo ndiyo maana huitwa Roho wa neema (Ebr.10:29). Ndiye anayefanya neema iokoayo ya Kristo ipate matumizi kwa wanadamu. (1Kor.15:10; 2Kor.9:14; Yak.4:5, 6).

2. ***Huleta ukweli wa Kristo****:* Kristo alimwita Roho Mtakatifu Roho wa Kweli (Yoh.14:17; 15:26; 16:13). Jukumu lake jingine ni kutukumbusha aliyotuambia Kristo (Yoh.14:26) na kutuongoza kwenye kweli (Yoh.16:13). Ujumbe wake unamshuhudia Kristo (Yoh.15:26). Pia humtukuza Kristo kwa kuwa hutwaa ya Kristo na kutupasha habari (Yoh.16:13, 14)

3. ***Huleta kuwepo kwa Kristo:*** Yesu alisema ni bora aondoke ili Roho aje (Yoh.14:16, 17; Yoh. 16:17). Akiwa katika umbo la kibinadamu, Yesua asingeweza kupatikana mahali pote na wakati wote. Aliahidi kutokutelekeza watu wake (Ebr.13:5; Mt. 28:20). Kwa kutambua ukweli huo, Roho amepewa jina ambalo halijapata kutumika kwenye Agano la Kale, Roho wa Kristo (Filp.1:19). Kwa njia ya Roho Mtakatifu, Baba na Mwana hufanya maskani kwa wanadamu (Yoh.14:23)

4. ***Hongoza Shughuli za Kanisa:*** Kwa kuwa Roho Mtakatifu ndiye Msaidizi wa Kristo, ndiye aliongozaye Kanisa. Alihusika wakati wa Mitume, kwa kuomba na kufunga wakachagua Wamishenari (Mdo.13:1-4). Waliochaguliwa walikuwa wamejawa na Roho (Mdo.13:9, cf.
   52). Matendo yao yalithibitiwa na Roho (Mdo.16”6, 7). Paulo alionya Wazee wa Kanisa kuwa walichaguliwa na Roho (Mdo.20:28). Roho Mtakatifu alitatua mgogoro wa kanisa, “Imempendeza Roho Mtakatifu na sisi…” (Mdo.15:28).

5. ***Hulipa Kanisa Karama maalum:*** Roho Mtakatifu huwajaza watu wa Mungu karama maalum. Katika Agano la Kale, aliwajaa watu wa Mungu na kutenda maajabu (Amu.3:10; 6:34; 11:29; nk) na uwezo wa kutabiri (Hes.11:17, 25, 26; 2Sam.23:2). Roho alimjia Sauli na Daudi walipotiwa mafuta (1Sam.10:6,10; 16:13). Kwa watu wengine Roho aliwapa ujuzi maalum (Kut.28:3; 31:3; 35:30-35). Katika Kanisa la Awali, Roho Mtakatifu aligawa karama kadiri alivyoona yeye inafaa ili kazi ya utume itendeke na kulinufaisha kanisa zima (Mdo.2:38; 1Kor.12:7-14; Efe.4:11, 12) na kukamilisha utume wa injili (Mdo.1:8).

Hujaa kwenye mioyo ya Waumini: Kwa swali la Paulo, je mlipokea Roho Mtakatifu mlipobatizwa, jibu la la, lilimfanya kuwabatiza na waliobatizwa walijawa Roho Mtakatifu. (Mdo.192, 6). Yesu alizungumzia umuhimu wa kubatizwa kwa maji na kwa Roho (Yoh.3:5). Kabla ya kupaa, aliagiza ubatizo unapofanywa, ufanywe kwa Jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu (Mt.28:19). Petro anasema Roho Mtakatifu hupokewa wakati wa ubatizo (Mdo.2;38), jambo ambalo linathibitishwa na Paulo. (Efe.518). Roho hutubadilisha, tufanane na Mungu (Tit.3:5, 6). Roho ni muhimu katika maisha ya kikristo na pasipo yeye hatutaweza kufanya lolote. (Yoh.15:5).